

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BWIRU
SIMU 0623444900 P.O.BOX 170 MWANZA
BARUA PEPE bwirugirls@gmail.com

KUMB.BGSS/JIF/01/2022

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

.....

S.L.P

.....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BWIRU KWA
MWAKA WA MASOMO 2022/2023**

Mpendwa mwanafunzi.....


Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **TANO** mwaka wa masomo **2022/2023** katika shule ya Sekondari Wasichana Bwiru. Mwaka wa masomo utaanza tarehe **...../...../2022** na unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **...../...../2022**. Tafadhali ripoti mapema tayari kwa kuanza masomo.

Mahali shule ilipo

Shule ya sekondari ya wasichana Bwiru iko katika kata ya Pasiyasi, Manispaa ya Ilemela Mkoani Mwanza. Shule inafikika kiurahisi kwani kuna usafiri wa magari ya abiria(daladala) kutoka mjini hadi Bwiru. Magari hayo yanapatikana kwenye stendi ya Bwiru iliyoko karibu na soko kuu Mwanza mjini.

Pamoja na barua hii naambatisha orodha ya vifaa muhimu ambavyo lazima uwe navyo, sheria za shule, kanuni za shule ambazo unatakiwa uzifuate kwa muda wote utakaokuwa mwanafunzi wa shule hii, **cheti cha kuzaliwa kama hauna uje na Affidavit** . **Fomu ya uthibitisho wa afya yako iliyojazwa na daktari wa hospitali ya serikali tu**, fomu ya taarifa binafsi ambazo unatakiwa kuzikamilisha kabla hujafika shuleni, result slip/hati ya matokeo original na fotokopi pamoja na fomu ya kukubali nafasi ya shule.

Mzazi/mlezi na mwanafunzi, mnatakiwa kusoma/kujaza maelekezo hayo kwa makini ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza.

 HEADMISTRESS
Bwiru Girls Secondary School
MWANZA

Mecktilda J. Shija
MKUU WA SHULE

SHERIA ZA SHULE:

Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa asijihusishe na makosa yafuatayo hapa chini vinginevyo anaweza kufukuzwa shule

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji wa bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma au mali ya mtu binafsi
8. Kudharau Bendera ya Taifa/wimbo wa Taifa
9. Kuolewa
10. Kupata mimba
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule na jumuiya nzima.
13. Kukataa adhabu /kugomea adhabu
14. Kuingia kwenye vilabu vya pombe, nyumba za kulala wageni na katika kumbi za starehe
15. Kulala nje ya shule bila ruhusa
16. Utoro
17. Kutumia au kumiliki simu shuleni.

KANUNI ZA SHULE:

A.HESHIMA.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

1. Kusimama na kumsalimu Mwalimu/mfanyakazi au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano
2. Kutotumia lugha mbaya wakati wowote kwa wanafunzi wenzake, walimu/wafanyakazi na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wake.
4. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
6. Kuwa na kucha fupi zisizo pakwa rangi, na nywele fupi (kwa asiyependa kusuka) pia ziwekwe katika hali ya usafi kila wakati, kuvaa mavazi ya heshima.
7. Kuitika mara moja na kukimbia kuelekea aliko mtu anayekuhitaji (mwalimu/mfanyakazi/kirinja).
8. Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Serikali, Nembo ya Taifa "Coat of Arms", wimbo wa Taifa na fedha, za Taifa.

